

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TISA

19 JUNI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TISA TAREHE 19 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

629. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Bajeti ya Barabara za Wilaya ya Misenyi zenye mtandao wa Kilomita 921 itaongezwa ili barabara hizo zitengenezwe kwa ubora.

630. MHESHIMIWA DKT. FLORENCE GEORGE SAMIZI (MUHAMBWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Kibondo Mjini yenye urefu wa Km 6 kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MAJI:

631. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Kata sita za Wilaya ya Muleba.

632. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa huduma ya maji bure Vijijini kama ilivyo kwenye baadhi ya huduma za Elimu na Afya.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

633. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya Uvinza pamoja na Mahakama za Mwanzo Kalya na Buhingu.

WIZARA YA UJENZI

634. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itatenga fedha za Ujenzi wa Barabara ya Makofia - Mlandizi - Mzenga hadi Maneromango kwa kiwango cha lami.

635. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itafanyia ukarabati nyumba chakavu za TBA zilizopo Bagamoyo pamoja na kujenga nyingine ili Watumishi na Wateja waishi vizuri.

636. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Iguguno hadi Ndunguti - Mkalama itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

637. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Kiranjeranje - Nanjirinji hadi Ruangwa kwa kiwango cha lami utaanza.

WIZARA YA KILIMO:

638. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali inawasaidia vipi Wakulima ambao mazao yao yameharibiwa na mafuriko.

639. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatafuta Mwekezaji kwa ajili ya kilimo cha Miwa na Kiwanda cha Sukari katika Kata ya Mahenge Wilayani Kilolo.

640. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipangaje katika kuhamasisha Kilimo hai kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya chakula, nguo na vipodozi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

641. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa Vitambulisho vya Taifa Wafungwa pamoja na Mahabusu.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
19 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

